HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

MKOA WA ARUSHA
Barua zote ziandikwe kwa
Mkuu wa Shule
Simu na.+ 255 754 948 916
+255 786 921 183
+255 757 754 836

MESERANI SEKONDARI
S. L. P 8.
MONDULI
ARUSHA -TANZANIA

EDUCATION IS A KEY TO SUCCESS

KUMB. NA MOND/MESERANI/SS//JI/2024/01 12/12/2023

JINA LA MWANAFUNZI.……
SHULE ANAKOTOKA ……..……..

YAH:MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MESERANI WILAYA YA MONDULI MKOA ARUSHA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024

1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2024 katika shule ya Sekondari MESERANI. Shule ya Sekondari MESERANI ipo Mkoa wa Arusha Wilaya ya Monduli Kata ya MESERANI. Shule iko umbali wa km 10 kutoka Duka bovu uelekeo wa barabara yaLoksale. Usafiri wa bodaboda na bajaji unapatikana Duka bovu. Kwa wale wa karibu wanaweza kufika kwa miguu kwani shule ipo karibu na barabara kuu ya kwenda Lolkisale.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **08/01/2024**, unatakiwa kufika shuleni kuanzia tarehe **08/01/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2024** ndani ya siku 14, tangu shule ilipofunguliwa. Mwanafuzi asiporipoti shuleni hadi kufikia tarehe **22/01/2024**mzazi atakamatwa na kushitakiwa kwa kosa la kumnyima mtoto haki ya kusoma

muhimu:

1. Mwanafunzi aweke alama kwenye sare yake ya shule ili kupunguza wizi
2. Hakikisha sare zinafanana na sampuli iliyoambatanishwa na fomu hii ili kuepuka usumbufu, aidha soma maelekezo yote kwa umakini na fomu zote zijazwe kisha zirudishwe shuleni.
3. Fomu hii ni batili kama haina muhuri wa mkuu wa shule na sampuli za vitambaa vilivyoambatanishwa. Hairuhusiwi kutoa **Nakala (copy)** fomu hii.
4. Njoo na fomu hii ikiwa **HALISI** (Original) na ikiwa imejazwa vizuri fomu zote.
5. Fomu ya Daktari ijazwe na daktari aliyeidhinishwa katika hospitali ya Serikali baada ya mtoto kupimwa
6. Mwanafunzi asipofika shuleni ndani ya siku 14 mzazi atakamatwa na kushtakiwa.
7. Siku ya kuwaona watoto ni Jumamosi au Jumapili ya mwisho wa mwezi, wanaoruhusiwa kuwatembelea wanafunzi ni mzazi/mlezi halisi aliyeandikishwa shuleni tu. **Kama kuna ndugu au rafiki aambatane na mzazi wa mwanafunzi**

2. MAHITAJI YA MWANAFUNZI.

SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

i. Suruali mbili za heshima zisizobana yaani zisiwe "mnyonyo" Rangi ya damu ya mzee(maruni)**grade 1 (one**) isiyopauka kama sampuli ya kitambaa kilichoambatanishwa
ii. Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
iii. Sweta rangi ya **damu ya mzee (maruni**)shingo ya V na mkanda mweupe shingoni na mikononi. Rangi ya uzi imeambatanishwa.
iv. Soksi Rangi ya kaki jozi mbili
v. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba visivyochongoka
vi. Mkanda mweusi wa kawaida usio na urembo
vii. Suruali rangi ya **nyeusi** kwa ajili ya kushindia (kitambaa kimeambatanishwa)
viii. T-shirt ya **damu ya mzee (maruni**) kwa ajili ya kushindia. HIZI ZINAPATIKANA HAPA SHULENI ZIKIWA NA NEMBO YA SHULE KWA TSH.9000/=
ix. Traki suti rangi**damu ya mzee(maruni)aina ya tetroni** kwa ajili ya kushindia na usiku wakati wa kujisomea

B. WASICHANA

i. Sketi mbili za marinda za heshima rangi **damu yam zee (maruni) grade 1 (one)** isiyopauka kama sampuli ya kitambaa kilichoambatanishwa
ii. Shati mbili nyeupe mikono mifupi
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba visivyo na visigino virefu (viatu maarufu kama bajaji haviruhusiwi kabisa)
iv. Sweta rangi **damu ya mzee** shingo ya V yenye mkanda mweupe shingoni na mikononi, uzi umeambatanishwa.
v. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
vi. Sketi ya rangi **nyeusi** kwa ajili ya kushindia- shamba dress (kitambaa kimeambatanishwa)
vii. T.shirt rangi **damu ya mzee (maruni**) tetronikwa ajili ya kushindia. Isiwe mtumba na isiyo na maandishi yoyote –HIZI ZINAPATIKANA SHULENI KWA TSH. 9000/= ZIKIWA NA NEMBO YA SHULE.
viii. Traki suti ya rangi**damu ya mzee (maruni**) kwa ajili ya kushindia na usiku wakati wa kujisomea
ix. Hijab Nyeupe siyo kilemba au mtandio (kwa Waislamu tu)
x. Taulo za kike (Pedi) za kutosha

NB. *SARE ZOTE ZA SHULE ZITAWEKWA NEMBO YA SHULE MARA MWANAFUNZI ATAKAPORIPOTI SHULENI.NGUO NYINGINE ZOTE ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KABISA. UKIJA NAZO UTANYANG'ANYWA NA ZITACHOMWA MOTO*

3. VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI

i. Godoro moja la inchi mbili na nusu hadi tatu Aina ya **"TANFOAM**" Original (original linakuwa na muhuri wa moto) Zingatia maelekezo haya kuepuka usumbufu. **UKIJA NA AINA NYINGINE YA GODORO HUTAPOKELEWA**

ii. Blanketi**NZITO**

iii. Shuka mbili rangi ya pinki(wasichana) na bluu(wavulana)

iv. Sanduku la Bati ukubwa wa wastani

v. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko. Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kushiriki chombo cha chakula na mwenzake. Sahani, bakuli na kikombe viwe vya Alminium. Visiwe vya plastiki

vi. Mfuko imara (school bag) kwa ajili ya kubebea vitabu na daftari

vii. Karatasi (ream mbili) kwa ajili ya kufanyia mazoezi binafsi moja ya mistari(ruled paper) na nyingine isiyo na mistari(plain paper)

viii. Daftari kubwa 12 (**counter book Quire3)**, kalamu, penseli, na mkebe wa Hisabati (mathematical set). Madaftari yawe yamejaladiwa.

ix. Vifaa vya michezo kama vile bukta, t-shirt na raba rangi yeyote.

x. Rain boot (buti kwa ajili ya matope) kipindi cha mvua. **BUTI NI MUHIMU SANA**

xi. Kamusi ya kingereza Kwa kingereza (oxford dictionary)

xii. Vitabu vya masomo yote yanayosomwa hapa shuleni. Kiswahili, English, History, Geography, Mathematics, Biology, Civics, Chemistry, Physics na Literature in English

xiii. Taa za sola za kuchaji kwa jua. Shule bado haijafungiwa umeme.

xiv. Fefdha kwa ajili ya BIMA Tsh. 6000/=

xv. File moja kwa ajili ya kutunzia mitihani

MAHITAJI MENGINE YA MUHIMU

A. WAVULANA

i. Ufagio wa chelewa kwa ajili ya usafi

ii. Jembe moja

iii. Soft broom

iv. Ndoo mbili ndogo za lita 10 kwa ajili ya kuhifadhia maji na kufanyia usafi

B. WASICHANA

i. Ndoo mbili ndogo za lita 10 kwa ajili ya kuhifadhia maji na kufanyia usafi

ii. Fyekeo moja liwe limenolewa

iii. Rubber squizer moja

iv. Fagio za ukili

Karibu sana Meserani Sekondari

ELIESKIA G. MBWAMBO

MKUU WA SHULE

4. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazoagizwa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i. Kutunza mali za umma

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA MASOMO.

a. Wizi
b. Uasherati, usagaji na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
e. Kupigana au kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g. Kudharau bendera ya Taifa
h. Kuwa mjamzito/ kupata mimba/kutoa mimba/kumpa mwanafunzi mimba
i. Kuoa au kuolewa
j. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au jamii inayozunguka shule
k. Kukataa adhabu kwa makusudi
l. Kumiliki simu ya mkononi
m. Kuwekwa /kuweka kimada
n. Kuzurura ovyo kwenye nyumba za walimu

…….
ELIESKIA G. MBWAMBO
MKUU WA SHULE

5. FOMU MAALUMU YA TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI

Toa taarifa zifuatazo bila kuogopa na bila kushawishiwa na mtu yeyote

i. TAJA JINA LAKO KAMILI ……
ii. TAREHE YA KUZALIWA……
iii. URAIA……..
iv. JINSIA (ME/KE)……
v. SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA ……
vi. DINI YAKO ……
vii. KABILA LAKO……..
viii. UNAKOISHI (Kata/kijiji)……..
ix. UNAISHI NA WAZAZI WAKO WOTE? TIKI MOJAWAPO

Naishi na wazazi wote wawili ☐ Naishi na baba tu ☐ Naishi na mama tu ☐

Wazazi wangu wote hawapo hai. Hivyo naishi na ndugu wengine ☐

Taja mtu unayeishinaye na uhusiano kama haushi na wazazi…… mahusiano……

x. TAJA CHAMA, SHIRIKA, KIKUNDI CHA DINI AU JUMUIYA INAYOKUFADHILI KAMA IPO……..
xi. KATIKA MAISHA YAKO UNGEPENDA KUWA NANI? (mfano, daktari wa binadamu, mwalimu, mhandisi wa ujenzi, mwandishi wa habari, rubani, nahodha, daktari wa mifugo, afisa wanyama pori nk)……
xii. TAJA KARAMA YAKO (TALENTS) YAANI KITU ULICHONACHO YA KIPEKEE KATIKA MAISHA YAKO……..

xiii. ORODHESHA MICHEZO UNAYOPENDA UKIANZIA NA ULE UNAOPENDA ZAIDI
…… …… ……

xiv. TAJA NDUNGU ZAKO WAWILI WA KARIBU AMBAO WANAWEZA KUKUTEMBELEA SHULENI
1…… 2……

xv. JE UMEWAHI KUOTESHA MTI? ……
xvi. JE UNAPENDA MAZINGIRA? ……NA UNGEPENDA KUPEWA MTI WA KUTUNZA UKIFIKA SHULENI? ……

6. MAWASILIANO:

Taja namba za simu zinazopatatikana na kama kuna namba zaidi ya moja hasa za wazazi zote ziandikwe.

Unakumbushwa pia kama mzazi ukibadilisha namba siku ya mwanao anaporipoti shuleni hakikisha unampatia mwanao namba mpya.

Mawasiliano ya shule Angalia nembo ya shule hapo juu.

I. Jina la Mwenyekiti wa serikali ya Mtaa utokako……

Namba ya simu ya mwenyekiti……

II. Jina la Balozi wa mtaa……

Namba ya simu ya Balozi……

III. Jina la baba/mlezi……

Namba ya simu……

IV. Jina la mama/mlezi……

Namba ya simu……

V. Taja Ndugu wawili wa karibu:

1. Jina……..

   Namba ya simu…….

2. Jina……..……..…

   Namba ya simu…….

UTHIBITISHO

Mimi …… (Jina la mwanafunzi) Ninathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi na nakubaliana na sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Ninaahidi kuwa nitatii kwa muda wote nitakapokuwa shuleni na endapo nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule niko tayari kuadhibiwa kulingana na taratibu za shule.

Jina kamili la mwanafunzi…… saini……tarehe……

Jina la mzazi/mlezi……Saini……tarehe……

Uthibitisho wa mwalimu wa Usajili/Nidhamu shule ya Sekondari MESERANI

……

……

Saini ……..tarehe……..

AHADI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MALEZI YA MWANAE

(ijazwe na mzazi /mlezi wa mwanafunzi na kuiwasilisha shuleni)

Mimi…… ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi

……

Ninaahidi kumhudumia mwanangu na kumpatia mahitaji yake kwa wakati na kushirikiana na shule kumlea mtoto huyu. Aidha ninaahdi kwamba nitahakikisha mwanangu anasoma na kuhitimu kidato cha nne na hivyo sitakubaliana na utoro wa aina yoyote. Nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha mwanangu wa **KIKE** hatapata **UJAUZITO** wala sitamwoza au kupokea mahari wakati wote wa masomo yake. Endapo nitakiuka ahadi hii hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Saini ya

mzazi……Tarehe……simu…….

HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI

MKOA WA ARUSHA
Barua zote ziandikwe kwa
Mkuu wa Shule
Simu na. +255 754 948 916
+255 786 921 183
+255 757 754 836

MESERANI SEKONDARI
S. L. P 8.
MONDULI
ARUSHA -TANZANIA

EDUCATION IS A KEY TO SUCCESS

Ref: No. MOND/MES/SS/J. K1/2024/01 12/12/2023

(**PART A :**)

MEDICAL OFFICER ……

RE: REQUEST FOR EXAMINATION TO ……

Please examine the above named as his/her physical and mental fitness for full time schooling course. The examination should include the following categories (i – iii) each category or sub category of which will render ineligible in case of defect. Pregnancy (category viii) will also render a girl candidate ineligible to the course

……

THE HEAD MASTER

PART B

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/ unfit and mentally fit/ unfit for full time schooling course

PHYSICAL HEALTH

i. Eye ……..
ii. Hearing ……..
iii. Limbs ……
iv. Leprosy ……..
v. Epilepsy……..
vi. Neuroses ……
vii. Other serious diseases ……
viii. Pregnancy ……
ix. Any other comments regarding your examination ……
……

Station …… Designation……

Signature (Official Stamp) …… Date ……